# ZABURI

## Zb136/ Siku ya Mungu ya Nne ya kwarezima Mwaka B

**Musique: GRACE MUSHAGALUSA Fabrice**




1. Kando ya mito ya Babiloni,
   ndiko tulikokaa, na kulia machozi,
   tulipokumbuka sioni; katika miti iliyokuwako;
   tulitundika vinubi vyetu.

2. Maana huko waliotuhamisha
   walituomba nyimbo,
   waliotusumbua, furaha:
   Haya, tuimbieni wimbo wa sioni.

3. Tuimbeje wimbo wa Bwana
   katika nchi ya kigeni?
   Nikikusahau, ee yerusalemu,
   mkono wangu wa kuume na usahaliwe.

4. Ulimi wangu uambatane kaakaani mwangu,
   nisipokumbuka wewe,
   nisipoweka yerusalemu
   juu ya furaha yangu yote.